KISWAHILI
SEHEMU YA KWANZA:LUGHA
Muda: Saa 1 Dakika 40.

Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.

Maridhia alikuwa ameumbwa akaumbika. Sifa za urembo wake zilikuwa zimeenea kijijini ___1___ huko Twapambazuka. ___2___ urembo wake alikuwa na maneno matamu ya kumtoa nyoka pangoni. Kiburi ___3___ lilikuwa jambo la ___4___. Yeyote aliyemwomba ___5___ alijipata akimpongeza licha ya ombi lake ___6___.

1.	**A.** chote	**B.** mote	**C.** pote	**D.** kote
2.	**A.** Licha ya	**B.** Zaidi ya	**C.** Kando ya	**D.** Nyuma ya
3.	**A.** lake	**B.** chake	**C.** kwake	**D.** yake
4.	**A.** mwiko	**B.** kawaida	**C.** desturi	**D.** mila
5.	**A.** posa	**B.** mkono	**C.** harusi	**D.** bibi
6.	**A.** kutiliwa maanani	**B.** kutiwa kapuni	**C.** kupewa kipaumbele	**D.** kutiliwa mbangu

Kutiwa damu yenye virusi vya ukimwi ni mojawapo ya njia ___7___ kusambaza maradhi haya. Madaktari wamefanya ___8___ kutafuta dawa mujarabu ya kukabiliana na maradhi ___9___. ___10___ juhudi zao kufikia sasa ___11___. Wasife moyo maadamu ___12___. Wakenya wajue kuwa ugonjwa huu ___13___ Wakenya peke yao bali pia uchumi wetu. Vijana wenye nguvu za ___14___ mali ndio ___15___ sana na ukongo huu.

7.	**A.** inalotumiwa	**B.** inayotumiwa	**C.** inazotumiwa	**D.** zinazotumiwa
8.	**A.** liwe liwalo	**B.** kufa kuzikana	**C.** juu chini	**D.** juu kando
9.	**A.** hizi	**B.** hii	**C.** haya	**D.** huu
10.	**A.** Vilevile	**B.** Kwa hivyo	**C.** Hivyo basi	**D.** Hata hivyo
11.	**A.** zimefua dafu		**B.** zimegonga mwamba	
	C. zimeenda sambamba		**D.** zimepiga hatua	
12.	**A.** moyo wa mtu ni gongo la msitu		**B.** moyo wa kupenda na kuwiza huwa	
	C. akipenda chongo huita kengeza		**D.** mja hatindi rehema ali hai duniani	
13.	**A.** unawaua	**B.** umewama	**C.** utawaua	**D.** hauwaui
14.	**A.** kuzalisha	**B.** kushibisha	**C.** kutoza	**D.** kupata
15.	**A.** wanaadhirika	**B.** wameathirika	**C.** huadhirika	**D.** hufaidi

Compiled and supplied online by Schools Net Kenya | P.O.Box 85726-00200, Nairobi. Tel:+254202319748 | +254733836593 | email: infosnkenya@gmail.com. Order answers online at: www.schoolsnetkenya.com

*Kutoka swali la **16** mpaka **30**, chagua jibu sahihi.*

16. **Wao walimsifu kiongozi wao aliyetoka ng'ambo.**

Tambua mancno yaliyopigiwa kistari.

A. Nomino, kivumishi, nomino

B. Kiwakilishi, kivumishi, kielezi

C.Nomino, kiwakilishi, kielezi

D. Kivumishi, kielezi, nomino

17. Chagua sentensi yenye kitenzi - jina

A. Kuimba kwenu kutamfanya msaidiwe sana.

B. Utundu wake hauna faida yoyote.

C. Umati wa watu ulikusanyika katika ofisi.

D. Gae huwa chombo wakati wake.

18. Ni sentensi ipi iliyo na kiunganishi sahihi?

A. Licha ya nyumba kuwa ndogo iliwatoshea wageni wote.

B. Nisaidie na lau shilingi kumi ninunue keki

C. Bali na kuwa daktari Petero ni mwalimu wa chekechea.

D. Alimwua simba minghairi ya swara mzee?

19. Chagua sentensi yenye kielezi cha wakati.

A. Walipofika mapema walianza kukata nyasi uwanjani.

B. Hapa penu shambani hamna umeme.

C. Aliadhibiwa kwa mujibu wa sheria zilizowekwa.

D. Mama hututembelea mara sita kwa wiki.

20. Chagua sentensi inayoonyesha - na - ya kuonyesha mtendaji.

A. Mkulima analima kondeni penye magugu.

B. Wachezaji watashindana wao kwa wao.

C. Refa ana ujuzi wa kutosha kuuchezesha mchezo huo.

D. Wanafunzi watashauriwa na mwalimu wao.

21. **Kanusha**

Picha iliyofutwa itachorwa tena.

A. Picha ambayo haikufutwa haitachorwa tena.

B. Picha ambayo haikufutwa itachorwa tena.

C. Picha iliyofutwa, haitachorwa tena.

D. Picha haikufutwa wala haitachorwa tena.

22. Chagua sentensi iliyonyambuliwa katika kauli ya kutendesha.

A. Askari walimkimbisha mwizi kwa hasira.

B. Waliamua kututembesha katika bustani ya Uhuru.

C. Jaji alimtoza mhalifu faini ya shilingi milioni sita.

D. Umati wa watu ulidumiza amani katika mkutano wa kisiasa.

23. Geuza katika usemi wa taarifa.

"Nitaenda kwake kesho asubuhi," alisema.

A. Alisema kwamba nitaenda kwake kesho asubuhi.

B. Alisema kuwa angeenda kwake asubuhi ya siku iliyofuata.

C. Alimwambia kuwa angeenda kwake kesho.

D. Alisema kuwa angeenda kwake asubuhi ya siku iliyotangulia.

24. Chagua sentensi iliyo katika hali timilifu.

A. Mwanafunzi aliandika insha kisha akampelekea mwalimu asahihishe.

B. Timu hiyo haijacheza jinsi nilivyotarajia.

C. Paka huwanyonyesha wanawe msimu wa baridi kali.

D. Mwanafunzi asomaye na kujifunza mengi hufaulu kila wakati.

25. Ni sentensi gani yenye kielezi kinachoelezea kivumishi?

A. Daktari alimtibu vyema mgonjwa huyo.

B. Tulishangilia vizuri sana baada ya ushindi.

C. Mwalimu shupavu mno atapongezwa kwa bidii zake.

D. Mtoto huyo ni mtukutu kama baba yake.

Compiled and supplied online by Schools Net Kenya | P.0.Box 85726-00200, Nairobi. Tel:+254202319748 | +254733836593 | email: infosnkenya@gmail.com. Order answers online at: www.schoolsnetkenya.com

26. 'Chereko' ni jina lenye sauti ngapi?
A. 3
B. 6
C. 4
D. 7

27. **Tegua kitendawili kifuatacho.**
Ingawa sina mbawa naruka kama ndege.
A. Kuku
B. Tiara
C. Mbuni
D. Nyani

28. Ni tamathali gani iliyo na maana ya kuwa na wivu?
A. Inda ya joka la mdimu.
B. Ulimi kama upatu wa gungu.
C. Tukutu kama mwanaharamu.
D. Waka kama taa ya umeme.

29. Ni maelezo gani sahihi?
A. Kibafute - Ni mchezo wa watoto wa kijificha na kutafutana.
B. Gungwi - Ni mchezo wa kushindana nguvu katika kuvuta kamba baina ya pande mbili.
C. Kodwa - Ni mchezo wa watoto wa kurusha vijiwe na kuvitoa mashimoni.
D. Kibemasa - Ni mchezo wa kurushiana ngumi.

30. Tambua umbo hili.

A. Tao
B. Kopa
C. Duaradufu
D. Hilali

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali **31** mpaka **40**.*

Mimi na mwenzangu Puza tulikuwa tukielekea studioni ili kutayarisha taarifa za habari za siku hiyo. Kwa kuwa muda ulikuwa umeyoyoma sana, ilibidi tuharakishe. Mbele yetu palikuwa na mkururo wa watoto waliokuwa wakiukimbiza mpira wao. Hawakuonekana kujali wala kushughulika kuwa walikuwa wakichezea barabarani. Moyoni kuona hivyo, nilishikwa na wasiwasi ambao singeelezea asili yake.

Puza aliyenitangulia aligeuka na kunitupia jicho la kunikengemeka kwa kutembea aste aste. Hakuelewa kwa nini sikuona vile tulivyokuwa tumebanwa na wakati. Nilijaribu basi kuharakisha na nusura nijikwae. Hapo ndipo tuliposikia sauti kali kama puto lililopasuliwa. Kimya cha kaburi kilitanda. Muda si muda tulisikia usiahi mkali kutoka sehemu ya nyuma. Tuliangaliana kwa sekunde kadha kabla ya kugeuka na kutimua mbio kuelekea sehemu hiyo. Hamna aliyewazia tena utayarishaji wa taarifa ya habari.

Ghafla kama mauti, gari dogo lilipita kwa kasi ya umeme. Gari lenyewe lilitifua ghubari kubwa la vumbi; tukashindwa kusogea ila kubakia kukohoa kwenye wingu hilo kubwa. Hali ilipotulia, tulielekea pale palipokuwa na watoto wakicheza. Pale katikati alilala mtoto mmoja. Wengine walishindana kutuelezea yale yaliyotokea. Ilikuwa vigumu sana kujua tumsikilize nani hasa katika tirivyogo hiyo ya sauti.

Nilimzoa yule mtoto na kutimua mbio kuelekea palipokuwa na maegesho ya teksi. Watoto kadha wakanifuata nyuma. Hapo ndipo nilipomwita Puza tushughulike pamoja. Alidinda na badala yake aliingia mfukoni na kunikabidhi shilingi elfu mbili. Sikuridhika. Nikamwambia kuwa mambo ya pesa ni baadaye. Naye kuona hivyo, akaniambia. "Mimi nimekupa mchango wangu unaohitaji. Unataka nini zaidi? Mimi niliachana

naye na kupiga misamba mirefu. Nilikuwa na bahati kama mwana aliyezaliwa siku ya Ijumaa. Dereva mmoja wa teksi aliponiona, alifungua mlango haraka haraka. Nilijitoma ndani na yule majeruhi. Mtoto mmoja aliyeweza kunifikia aliingia ndani na teksi nayo ikavurumishwa kuelekea hospitalini.

Majeruhi wangu alianza kutetemeka kwa kuvuja damu. Damu ilikuwa bado inachuruzika. Hatimaye tuliwasili hospitalini. Wakuu wa pale walishikilia tulipe arbuni kwanza ili mtoto atibiwe. "Nyie namna gani? Maisha na arbuni kipi cha maana?" Hatimaye manesi waliokuwa pale walimbeba wanguwangu yule mtoto na kumwingiza ndani kwa matibabu. Mimi nilibaki pale kitini pamoja na yule mtoto aliyeandamana nami.

Nikiwa pale akili yangu iliduru huku na huko. Nilishangaa kama kweli wenyewe tuliwazia umuhimu wa schemu za watoto kuchezea. Ajali ilipotokea nyumba zilipangana bega kwa bega bila kuacha nafasi ya kuchezea.

Watoto walilazimika kuchezea barabarani kwa kukosa namna nyingine. Katika mawazo yangu hayo, nilikuja kugundua kuwa viwanja vyote vya kuchezea vilinyakuliwa na mabwanyenye waliojijali wao. Na hapo ndipo nilishindwa na kujiuliza, "Ikiwa mabwanyenye hawa wanawalea wana wao kwa tunu na tamasha, wasijue maana ya msamiati wa kukosa, kwa nini basi hawangeacha hata nafasi ya wana wao kuchezea?

'Ah! Kwa bahati hakuumia sana. Bega lake limeteguka na alichumbuliwa kichwani, kapoteza fahamu kwa sasa," niligutushwa na maneno ya daktari aliyevaa joho jeupe na kuning'iniza stethoskopu kifuani.

---

31. Kwa mujibu wa makala haya, msimulizi na mwenzake,
A. waliharakisha ili kusoma taarifa za habari za siku hiyo.
B. walipumbazwa na mpira uliokuwa ukichezewa barabarani.
C. walitabiri ajali iliyotokea baadaye.
D. walikuwa wanahabari katika studio moja.

32. Ni kweli kusema kuwa,
A. msimulizi alikuwa na mwao kuwa kulikuwa na ajali ambayo ingetokea.
B. taarifa za habari siku hiyo zilisomwa zikiwa zimechelewa.
C. usiahi uliotokea ulimfanya msimulizi na mwenziwe wasiwe wanahabari tena.
D. usiahi uliotokea, ulimfanya msimulizi na mwenzake kuachana na shughuli ya siku hiyo.

33. Watoto waliokuwa wakicheza,
A. walishuhudia ajali iliyompata mmoja wao.
B. hawakujua iwapo mwenzao alikuwa ameumia katika ajali iliyotokea.
C. walilishambulia gari dogo kwa mawe mpaka likatoroka.
D. walikuwa wamepanga kulishambulia gari dogo lililosababisha ajali.

34. "Mimi nimekupa mchango wangu uliohitaji. Unataka nini zaidi? Inaonyesha kuwa
A. msimulizi alimtarajia Puza kufikiria ajali ipasavyo.
B. msimulizi alimtarajia Puza kushirikiana naye kwa ukamilifu katika shughuli iliyowapata.
C. msimulizi alimtarajia Puza kuandamana naye hadi studioni.
D. msimulizi aliutarajia uelekezi ufaao kutoka kwa Puza.

35. "Nyie namna gani? Maisha na arbuni kipi cha maana?" Ni methali gani inayowcza kusimamia kauli hii?
A. Kata pua uunge wajili.
B. Ondoa dari uczeke paa.
C. Fisi akimla muwele, mzima funga mlango.
D. Kitu kilivunja mlima na nguu kulala.

36. Mwandishi aligundua ni nini hasa kilisababisha ajali kulingana na aya ya sita?
A. Gari dogo
B. Tamaa na ubinafsi
C. Barabara
D. Dereva

37. Arbuni ni ?
A. malipo kwa mganga.
B. malipo aliipaye majeruhi baada ya ajali ya barabarani.
C. Sehemu ya malipo yanayolipwa kwanza ili pesa zilizosalia zilipwe baadaye.
D. Malipo ya kwenda kumwona mgonjwa.

38. Mwisho wa makala haya unaonyesha kuwa,
A. msimulizi alihuzunishwa sana na kutelekezwa kwa mahitaji ya watoto na mabwanyenye.
B. msimulizi hakujali maslahi ya watoto hata kidogo.
C. Puza hakuclewa ni vipi matajiri wapatie pesa kipaumbele badala ya maisha ya watoto.
D. Puza hakusaidia kwa chochote katika changamoto mpya iliyozuka.

39. Wanawalea watoto wao kwa tunu na tamasha, wasijue maana ya msamiati wa kukosa. Usemi huu una maana gani?
A. Watoto wao walipendwa na kushauriwa jinsi ya kucheza.
B. Watoto wao walipendwa na kuonyeshwa yaliyowafaa katika maisha yao.
C. Watoto wao walipendwa na kurithishwa yote waliyoyataka.
D. Watoto wao waliopendwa na kutimiziwa mahitaji yao yote.

40. Ah! Ni tamathali gani ya lugha?
A. Kihusishi.
B. Kiigizi.
C. Kihisishi.
D. Kielezi.

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali **41** mpaka **50**.*

Vijana wa zamani walienzi na kuithamini michezo kama kito. Wazazi walikuwa na kibarua kigumu cha kuwarudisha watoto nyumbani. Vijana hawa waliicheza michezo mingi kwa mfano gungwi, kibe, kibafute, kuvutana kwa kamba, kuzungusha tairi kwenye kiuno na hata kuruka kwa kamba. Ilikuwa muhali kuwapata wana walionenepa kama hanziri.

Nao wenzao wa kisasa, tofauti yao na wao ni ile ya maji na mafuta. Asilimia kubwa badala ya kwenda nyanjani kucheza, hujikalia ubwana. Lao ni kupiga soga kuzihusu timu za ughaibuni.

Michezo inayo manufaa yasiyokadirika. Natumai unafahamu kuwa michezo husaidia kujenga misuli na kuimarisha viungo vya mwili. Ni wazi kuwa wakati unaposhiriki michezo, unajihisi mwepesi zaidi na unaweza kutekeleza mengi bila kuhisi kuchoka haraka. Pia kwa wale wanaoshiriki michezo katika ngazi za kimataifa hunufaika kwa mengi. Wao huambulia fedha nyingi na kuambulia utajiri wa haraka. Wengine huajiriwa kama makocha na marefa wa timu za kimaeneo, kitaifa au hata kimataifa

Husemekana kuwa akili vivu ni karakana ya maovu. Wale wanaojikalia shambiro bila kufanya kazi yoyote hujipata wakiyawazia mabaya. Kunao ambao watazama katika matumizi ya dawa za kulevya au wanaswe na mtego wa mapenzi kabla ya ndoa. Hata hivyo yule anayeshiriki katika michezo huwa hana nafasi ya kuyawazia mawi. Atokapo uwanjani huwa amechoka tiki na kukosa zihi za kufanya mawi.

Kulingana na uchunguzi uliofanywa na mtaalamu Brandly, wanafunzi wengi wanaoshiriki katika michezo huwa werevu masomoni. Michezo hukuza kumbukumbu za aliyosoma. Kumbuka uwanjani lazima mchezaji awe mmakinifu na anayechemsha bongo na kukuza ubunifu. Mwanafunzi kama huyo huwa na kichwa chepesi.

Fauka ya hayo michezo huchangia pakubwa katika kudumisha nidhamu. Michezo mingi huwa na sheria za kuudhibiti mchezo wenyewe. Wale ambao huvunja sheria hizi hupewa adhabu kali. Lazima kila mwanafunzi azifuate la sivyo atajiuma kidole. Michezoni lazima pawe na heshima kwa waelekezi na wachezaji wote. Adhabu wanazopewa wasiofuata sheria zilizowekwa huwaadilisha na kuwalainisha.

Michezo vilevile hukuza stadi muhimu maishani. Stadi hizi ni ujasiri wa kumenyana na mazito, bidii, uvumilivu na stahamala, ushirikiano, kulenga shabaha na kusuluhisha migogoro. Demokrasia nayo hukuzwa katika uchaguzi wa wachezaji na timu. Isitoshe uongozi hutambuliwa na kuendelezwa kwa kuchagua vinara na manahodha wa timu mbalimbali. Vilevile wachezaji hufunzwa kuyakubali matokeo ya ushindi na ushinde. Hii hujikita katika msingi wa asiyekubali kushindwa si mshindani.

Zaidi ya yote, michezo pia huwatangamanisha watu wa matabaka mbalimbali, jamii na jamaa za mbali na karibu. Mipaka ya kikabila, kitabaka au hata kimaeneo huwekwa kando. Hali hii huleta uwiano na maendeleo ya hali ya juu.

---

41. Ni lipi linaloonyesha kwamba vijana wa zamani waliipenda michezo?
A. Wao waliicheza michezo mingi ikilinganishwa na wenzao wa siku hizi.
B. Vijana wa zamani waliithamini michezo ya riadha kuliko aina nyinginc ile.
C. Wazazi wa vijana wa zamani walikuwa na kazi ngumu ya kuwarudisha watoto nyumbani.
D. Vijana wa zamani hawakuneneпa kama nguruwe.

42. Tofauti baina ya vijana wa kisasa na wa zamani ni kuwa,
A. vijana wa leo wanathamini michezo sana.
B. vijana wa zamani hawakuthamini michezo hata kidogo.
C. hakuna tofauti hata kidogo kwa kuwa mitazamo yao ilikuwa tofauti.
D. vijana wa kisasa hawathamini sana michezo.

43. Kulingana na aya ya tatu,
A. vijana wote hunufaika na kuithamini michezo.
B. vijana wanaoshiriki michezo hupata utulivu zaidi wa mwili.
C. misuli huimarika mtu anapofahamu umuhimu wa kucheza.
D. viungo hujengeka michezoni mtu anapofanya kazi kwa urahisi.

44. Chagua kauli ya kweli kulingana na kifungu.
A. Vijana hupenda kuamka asubuhi na mapema kuelekea uwanjani.
B. Manufaa ya michezo kwa vijana huanzia nyumbani.
C. Vijana wakichezea timu za kimataifa wao huweza kuajiriwa.
D. Kushiriki michezo huweza kuimarisha hali ya mtu kiuchumi.

45. Michezo
A. huondoa hamu ya kuoa na kutumia dawa za kulevya miongoni mwa vijana.
B. huchosha vijana mpaka wanashindwa kutafuta wapenzi na dawa za kulevya.
C. huwasaidia vijana kujiepusha na maovu ya kijamii.
D. ndiyo dawa mujarabu kwa watumiao dawa na kufunga ndoa za mapema.

46. Michezo hukuza demokrasia
A. katika kuchagua viongozi wa timu.
B. katika kuwatangamanisha watu.
C. katika kuchagua wafadhili wa timu.
D. katika kudumisha nidhamu ya wachezaji.

47. Michezo
A. inapowaleta watu pamoja idadi ya vijana huwa nyingi uwanjani.
B. ikiimarisha nidhamu idadi ya wachezaji huongezeka.
C. inawafanya watu kuwa na moyo wa kukabiliana na magumu.
D. husababisha kuwako kwa mashabiki wanaowapenda vijana.

48. Kulingana na mtaalamu Brandly,
A. wachezaji wote ambao hushiriki katika michezo huwa werevu.
B. michezo huchangia pakubwa katika kunoa akili.
C. bora kijana ashiriki michezo, atakuwa mwerevu.
D. michezo ndiyo njia ya pekee ya kuwa mwerevu darasani.

49. Kulingana na aya ya mwisho,
A. michezo huweza kupunguza pengo baina ya walalahoi na matajiri ifikapo ni kushabikia timu.
B. michezo hukuza na kupalilia ukabila na maovu mengine ya kijamii.
C. michezo huchangia katika kutenganisha wakazi wa matabaka mbalimbali.
D. michezo ina uwezo wa kukufaa kiuchumi iwapo utamakinika.

50. Kulingana na kifungu, <u>yasiyokadirika</u> ina maana ya
A. yasiyofikirika
B. yasiyowezekana
C. yasiyokisika
D. mengi